

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
29 machi 2008**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kibwana Mohammad Msiga
Paulo Atibu Hatibu
Sosthenes C Amlima
Sudi Saidi Ramadhan

Ofisi, guta na mambo ya fedha

Wakati wa wiki Ally Saidi Mohammed alipeleka bao ya tangazo ofisini na aliweka ukutani, basi sasa kuna nafasi kubwa ya matangazo. Juma alinunua kamba zaidi kwa rafu kwa Tsh 1,000. Juma alimrudisha Ally Saidi Mohammed hela yake ya Tsh 5,000 ambaye alitumia kusafirisha bao kwa pick up. Elaine alisema ni muhimu kupata resiti, hata kama resiti ni karatasi ya kawaida tu ambayo imesainiwa na aliyepokea hela. Ally Saidi Mohammed alisema ni muhimu kwamba matumizi ya fedha na balance ya UWABA's itangaze kwenye kila mkutano. Tulikadiri kwamba balance ya benki sasa ni Tsh 368,000. Ally Saidi Mwishehe alileta Tsh 7,000 ya hela ya guta. Juma sasa ana Tsh 26,000 ya hela ya UWABA nyumbani kwake.

Uzinduzi wa ofisi

Tulikubali kuwa na uzinduzi wa ofisi jumamosi tarehe 19 Aprili saa nne asubuhi.

Wiki jana tulifanya orodha ya watu kuwaalika kwenye uzinduzi wa ofisi na wiki hii tuliongeza majina ya Mhe Azzan Zungu, mwakilishi wa kata ya Mabibo, Ubalozzi wa Uholonzi, SUMATRA, TABOA na polisi wa trafiki.

Tulikubali kumwomba Dominata kuwasiliana na waandishi wa habari.

Tulikubali kuandika barua ya kuomba kibali cha kutumia mtaa nje ya ofisi kwenda mwenyekiti wa mtaa Jitegemee.

Ally Saidi Mohammad alipata mtu anayekodisha vifaa vya musiki anayeitwa Charles ambaye alikuja kwenye mkutano. Alikubali kukodisha vifaa kwa Tsh 30,000, na tulikubali kumpa advance ya Tsh 20,000 wiki ijayo. Paulo na Filbert watafanya utafiti kuhusu vipi kukodi hema. Tutaomba Maktaba bar kutupa viti na tutanunua soda kutoka kwao. Tutawaomba kutupa generator kama umeme umekatika. Tatalipa Tsh 5,000 Luku ya gharama ya umeme kwa Ally Saidi Mohammed's kutumia umeme wa nyumba yake kama umeme haujakatika.

Ally Saidi Mohammed na Sosthenes walipendekeza tutoe nakala ya hotuba na vipeperushi kwa wageni kwenye uzinduzi.

Markus Weise

Elaine alisema kwamba Markus Weise, mwanafunzi wa Ursinus College, Pennsylvania Merekani, atakuwepo Dar es Salaam kufanya utafiti kuhusu masuala ya baisikeli kwa kipindi cha miezi miwili au mitatu. Atapenda kushirikiana na UWABA na kutusaidia katika miradi yetu. Anafanya mradi huu chini ya Watson Fellowship. Atafika mwishoni wa Aprili. Tayari amefanya utafiti huu Namibia, Bangladesh na Vietnam.

Wamba Memorial Fund

Hatujapata jibu kwa email au message ya simu kutoka Wamba memorial fund. Elaine alijaribu kutumia email kwa anwani za email mbali mbali.

Barabara ya Morogoro

Juma alipeleka barua TANROADS Dar es Salaam kuhusu vifuniko vya mifereji maeneo ya Jangwani barabara ya Morogoro. Aliongea pamoja na mkurugenzi wa TANROADS Dar es Salaam, ambaye alisema watarekebisha.

Maguta ya Ulaya

Elaine alionyesha picha kutoka Robert Bartlett za matumizi ya baisikeli za gurudumu tatu Ulaya.